Fataawaa al-Lajnah ad-Daaimah

´Abdul-´Aziyz bin Baaz
´Abdur-Razzaaq ´Afiyfiy
´Abdullaah bin al-Ghudayyaan
´Abdullaah bin Qu´uud

Tarjama na ufupisho:

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

Juzu ya tatu

YALIYOMO:

131. Imaam Ibn Baaz Kuhusu Kusherehekea Maulidi 5

132. al-Lajnah ad-Daaimah Kuhusu Kusherehekea Maulidi..... 12

133. Kusherehekea Maulidi Na Israa´ Na Mi´raaj Kwa Lengo Kudhihirisha Desturi Za Kiislamu 12

134. Kufanya Maulidi Ni Halali Au Haramu? 14

135. Kusherehekea Siku Ya 27 Ramadhaan 14

136. Kupika Chakula Usiku Wa Mi´raaj Na Laylat-ul-Qadr Na Kumtumia Thawabu Maiti 15

137. Imaam Ibn Baaz Kusherehekea Usiku Wa Israa´ Na Mi´raaj 15

138. Imaam Ibn Baaz Kusherehekea Usiku Wa Nifsu Sha´baan 19

139. Baba Ameacha Wasia Atolewe Swadaqah Kila Mwaka Nisfu Sha´baan 29

140. Kusoma Aayah Kwa Idadi Maalum Ili Mtu Apate Alichokipoteza..... 30

141. Kusema "Karrama Allaahu wajhah" Kwa ´Aliy Halina Asli 30

142. Kusoma Qur-aan Au al-Burdaa Wakati Wa Kwenda Kuzika 31

143. Maana Ya Kufuru Katika Sifa Za Allaah..... 31

144. Hadiyth Ya Mjakazi Kuhusu Allaah Kuwa Juu Ni Dhaifu? 32

145. ´Arshi Na Kursiy Viko Ardhini Au Mbinguni?..... 33

146. Imamu Wa Msikiti Anasema Kuwa Qur-aan Imetengenezwa 33

147. Mwenye Kufa Katika ´Aqiydah Ya Ashaa´irah 35

148. Imaam an-Nawawiy Asiigwe Katika Mlango Huu..... 35

149. Hukumu Ya Ta´wiyl..... 36

150. Idadi Ya Mitume Na Manabii Haijulikani 36

151. Kwanini Asikufurishwe Anayesema ´Aliy Ndio Mtume? 37

152. Mtume Alikuwa Macho Israa´ Na Mi´raaj? 37

153. Mtume Alipandishwa Mbinguni Kwa Roho Bila Ya Mwili Au Vyote Viwili? 38
154. Vipi Mtume Aliwaona Watu Motoni Na Qiyaamah Bado? 39
155. Mtume (´alayhis-Salaam) Anasahau? 39
156. Maswahabah Kumi Waliobashiriwa Pepo 40
157. Dini Ya Mayahudi Na Manaswara Haitowanufaisha Kitu 40
158. Kupokea Zawadi Kutoka Kwa Makafiri 40
159. Kumuombea Msamaha Maiti Aliyeritadi 41
160. Kuwaombea Msamaha Mababu Waliokufa Katika Shirki 42
161. Muislamu Kuanza Kumsalimia Kafiri 42
162. Maiti Humuona Mtume (´alayhis-Salaam) Kaburini? 43
163. al-Lajnah ad-Daaimah Kuhusu "as-Swahiyh" Ya al-Bukhaariy 44
164. Mtoto Wa Nje Ya Ndoa Ataingia Peponi? 45
165. Ibliys Ni Malaika Au Jini? 45
166. Qur-aan Au ´Iysaa (´alayhis-Salaam)? 47
167. Suurah Za Qur-aan Nani Alizipa Majina? 47
168. Kusoma Na Msahafu Au Bila Msahafu? 47
169. Kusoma Qur-aan Kwa Sauti Ya Juu Msikitini 48
170. Kuingia Na Msahafu Chooni 48
171. Inafaa Kumpa Kafiri Qur-aan Iliyotarjumiwa? 49
172. Kutumia Aayah Za Qur-aan Katika Mazungumzo Ya Kawaida 49
173. al-Lajnah ad-Daaimah Kuhusu Kusoma Qur-aan Bila Wudhuu 50
174. Kupokea Mshahara Kwa Kufunza Qur-aan 51
175. Msahafu Wa Zamani Unafanywa Nini? 51
176. Msahafu Uliochapishwa Makosa Unafanywa Nini? 52

177. Vitabu Vya Dini Visivyotumiwa Vinafanywa Nini? 52
178. Kusoma Qur-aan Na Huku Mtu Anafuatilia Mkanda 52
179. Kusoma Qur-aan Kwa Kushegama, Kusimama Na Kutembea 53
180. Inajuzu Kusoma Qur-aan Nyakati Swalah Imekatazwa? 53
181. al-Lajnah ad-Daaimah Kusoma Qur-aan Kwa Pamoja 54
182. Kwenda Kwa Mbele Na Kwa Nyuma Wakati Wa Kusoma Qur-aan 55
183. Kusema "Swadaqah Allaahu al-´Adhwiym" Ni Bid´ah 55
184. Kubusu Msahafu Ni Jambo Halina Asli 56
185. Inajuzu Kumsikiliza Mwanamke Anayesoma Qur-aan? 56
186. Inafaa Kwa Mwanamke Kusoma Kwa Sauti Ya Juu? 57
187. Mashindishano Ya Qur-aan Kwa Wasichana Mbele Ya Wanaume 57
188. Sunnah Ni Wahiy Kutoka Kwa Allaah 58



131. Imaam Ibn Baaz Kuhusu Kusherehekea Maulidi

Himdi zote anastahiki Allaah Pekee. Swalah na salaam zimwendee Mtume wa Allaah, kizazi chake, Maswahabah zake na wenye kufuata uongofu wake.

Amma ba´d:

Kumekuja maswali mengi yenye kukariri yanayouliza juu ya hukumu ya kusherehekea mazazi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kuyasimamia, kumtolea Salaam na mengineyo yanayofanywa katika Maulidi.

Jibu ni kama ifuatavyo: haijuzu kushereheka mazazi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wala ya mwingine. Kwa sababu hiyo ni katika Bid´ah iliyozuliwa katika dini. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakuyafanya, makhaliyfah wake waongofu, mtu mwengine katika Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) wala Taabi´uun yeyote katika karne bora. Watu hawa ni wajuzi zaidi juu ya Sunnah na wana mapenzi kamilifu kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wenye kufuata Shari´ah yake zaidi kuliko waliokuja baada yao. Imethibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

“Mwenye kuzua katika dini yetu hii yasiyokuwemo atarudishiwa mwenyewe.”

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika Hadiyth nyingine:

“Jilazimieni na Sunnah zangu na Sunnah za makhaliyfah wangu waongofu baada yangu. Shikamaneni nazo na mziume kwa magego. Tahadharini na mambo ya kuzua! Hakika kila kitachozushwa ni Bid´ah na kila Bid´ah ni upotevu.”

Katika Hadiyth hizi mbili kuna maonyo makali juu ya kuzua Bid´ah na kuitendea kazi. Allaah (Subhaanah) amesema katika Kitabu Chake chenye kubainisha:

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا

"Na lolote lile analokupeni Mtume na lolote lile analokukatazeni, basi acheni. Na mcheni Allaah." (59:07)

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

"Basi watahadhari wale wanaokhalifu amri yake, isije kuwasibu *fitnah* au ikawasibu adhabu iumizayo." (24:63)

لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا

"Kwa yakini mna kigezo kizuri kwa Mtume wa Allaah kwa mwenye kumtaraji Allaah na Siku ya Mwisho na akamdhukuru Allaah kwa wingi." (33:21)

وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُم بِإِحْسَانٍ رَّضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

"Na wale waliotangulia awali miongoni mwa *Muhaajiriyn* na *Answaar* na wale waliowafuata kwa wema Allaah Ameridhika nao nao wameridhika Naye. Na Amewaandalia mabustani yapitayo chini yake mito. Ni wenye kudumu humo milele - huko ndiko kufuzu kukuu." (09:100)

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

"Leo Nimekukamilishieni Dini yenu na Nimekutimizieni neema Yangu na Nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe ndio Dini yenu." (05:03)

Aayah zilizo na maana kama hii ni nyingi.

Kuzusha mazao kama haya kinachopata kufahamika ndani yake ni kuwa Allaah (Subhaanah) hakuukamilishia Ummah huu dini na kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakufikisha yale ambayo Ummah wanatakiwa kuyatendea kazi mpaka walipokuja hawa waliokuja nyuma na wakawa wamezua katika Shari´ah ya Allaah yale ambayo hakuyatolea dalili. Wamefanya hivyo na huku wanadai kuwa wayafanyayo yanawakurubisha kwa Allaah. Hili, bila ya shaka, ndani yake kuna khatari kubwa na ni

kupingana na Allaah (Subhaanah) na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Allaah (Subhaanah) amewakamilishia waja Wake dini na akawatimizia neema. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amefikisha ufikisho wa wazi. Hakuacha njia inamyofikisha mtu Peponi na kumuweka mtu mbali na Moto isipokuwa amewabainishia nayo Ummah. Imethibiti katika Hadiyth Swahiyh kupitia kwa ´Abdullaah bin ´Amr (Radhiya Allaahu ´anhumaa) ambaye ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Allaah hakutuma Mtume yeyote isipokuwa ilikuwa ni haki juu yake awaelekeze Ummah wake katika kheri anayoijua kwao na awatahadharishe na shari anayoijua kwao."

Ameipokea Muslim katika "as-Swahiyh" yake.

Ni jambo linalojulikana kuwa Mtume wetu (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndio Mtume bora kabisa, wa mwisho wao, mfikishaji na mnasihiaji mkamilifu zaidi. Lau kusherehekea Maulidi ingelikuwa ni sehemu katika dini ambayo Allaah (Subhaanah) anairidhia basi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) angeliwabainishia Ummah au angalau kwa uchache angelipatapo kuyafanya katika maisha yake au Maswahabah zake (Radhiya Allaahu ´anhum) wangeliyafanya. Pale ambapo hakukupatikana kitu katika hayo ndipo ikapata kujulikana kuwa Maulidi hayana lolote kuhusiana na Uislamu. Bali ni katika mambo yaliyozuliwa ambayo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameutahadharisha Ummah wake nayo, jambo ambalo tumetangulia kulisema katika Hadiyth mbili zilizotangulia. Kuna Hadiyth zingine zimekuja zikiwa na maana kama hiyo. Baadhi yazo ni maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika Khutbah ya Ijumaa:

"Amma ba´d: Hakika maneno bora kabisa ni Kitabu cha Allaah, uongofu bora ni wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), uovu wa mambo ni ya kuzua, hakika kila Bid´ah ni upotevu."

Ameipokea Imaam Muslim katika "as-Swahiyh" yake.

Aayah na Hadiyth juu ya mada hii ni nyingi.

Kuna wanachuoni ambao wameweka wazi kuyakemea Maulidi na kutahadharisha juu yake kwa kutendea kazi dalili zilizotajwa na nyinginezo wakati baadhi ya wengine waliokuja nyuma wakaenda kinyume na kuyajuzisha. Kwa sharti yakiwa hayana maovu yoyote. Maovu hayo ni kama kuvuka mipaka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), wanawake kuchanganyika na wanaume, kutumia ala za muziki na mengineyo ambayo yanapingwa na Shari´ah hii twaharifu. Wanachuoni hao walifikiria kuwa ni miongoni mwa Bid´ah zilizo nzuri. Kanuni ya Kishari´ah inasema kurudisha yale ambayo watu wametofautiana kwayo katika Qur-aan na Sunnah. Allaah (´Azza wa Jall) amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ ۖ فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا

"Enyi mlioamini! Mtiini Allaah na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi. Mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Allaah na Mtume mkiwa mnamwamini Allaah na Siku ya Mwisho. Hivyo ni [njia] bora na matokeo mazuri zaidi." (04:59)

وَمَا اخْتَلَفْتُمْ فِيهِ مِن شَيْءٍ فَحُكْمُهُ إِلَى اللَّهِ

"Na katika jambo lolote lile mlilokhitilafiana ndani yake, basi hukumu yake ni kwa Allaah." (42:10)

Tumeyarudisha masuala haya – ambayo ni kusherehekea mazazi ya Mtume – katika Qur-aan. Tumechopata kuona ni kwamba inatuamrisha kumfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika yale aliyokuja nayo na inatuonya na yale aliyokataza. Qur-aan inatukhabarisha kuwa Allaah (Subhaanah) ameukamilishia Ummah huu dini. Sherehe hii sio miongoni mwa yale aliyokuja nayo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hivyo hayana nafasi katika dini ambayo Allaah ametukamilishia nayo na kutuamrisha kumfuata Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika dini hiyo.

Hali kadhalika tumeyarudisha katika Sunnah na hatukupata kuona kuwa aliyafanya, kuyaamrisha wala Maswahabah zake (Radhiya Allaahu ´anhum) kuyafanya. Hayo yakatufahamisha kuwa sio katika dini. Bali kinyume chake

ni katika Bid´ah iliyozushwa. Vilevile isitoshe ni kujifananisha na mayahudi na manaswara katika sherehe zao.

Kwa hayo inapata kujulikana kwa kila ambaye ana ujuzi angalau kidogo na malengo yake ni haki na uadilifu katika kutafuta kwake ya kwamba kusherehekea Maulidi sio katika dini ya Uislamu. Kinyume chake ni katika Bid´ah zilizozuliwa ambazo Allaah (Subhaanah) na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wameamrisha kuyaacha na kutahadharisha nayo.

Haitakikani kwa mwenye busara kudanganyika na watu wengi wenye kuyafanya katika miji mbali mbali. Haki haijulikani kwa wengi wa wenye kuifanya. Haki inajulikana kupitia dalili za Kishari´ah. Allaah (Ta´ala) amesema juu ya mayahudi na manaswara:

وَقَالُوا لَن يَدْخُلَ الْجَنَّةَ إِلَّا مَن كَانَ هُودًا أَوْ نَصَارَىٰ ۗ تِلْكَ أَمَانِيُّهُمْ ۗ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ

"Na walisema: “Hatoingia Peponi isipokuwa aliyekuwa Yahudi au Naswara.” Hilo ni tamanio lao. Sema: “Leteni ushahidi wenu wa wazi mkiwa ni wakweli"." (02:111)

وَإِن تُطِعْ أَكْثَرَ مَن فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ

"Na kama ukiwatii wengi walioko ulimwenguni, watakupoteza na njia ya Allaah." (06:116)

Isitoshe jengine ni kuwa sherehe hizi za Maulidi, pamoja na kuwa ni Bid´ah, mara nyingi ndani yake hakukosi maovu. Baadhi ya maovu hayo ni kama wanawake kuchanganyika na wanaume, muziki na nyimbo, pombe na madawa ya kulevya na maovu mengineyo. Sivyo tu, bali kunaweza kutokea kubwa kuliko hayo. Nacho ni shirki kubwa kwa njia ya kuvuka mipaka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) au walii mwingine kwa kumuomba, kumtaka msaada na uokozi, kuamini kuwa anajua elimu ya mambo yaliyofichikana na mengineyo katika mambo ya kikafiri ambayo yanafanya watu wengi wakati wanaposherehekea mazazi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na ya wengine miongoni mwa wale wanaowaita kuwa ni “mawalii”. Imesihi kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

“Tahadharini na kupetuka mipaka katika dini. Hakika kilichowaangamiza waliokuwa kabla yenu ilikuwa ni kuvuka mipaka katika dini.”

Amesema tena (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

“Msinisifu kupindukia kama walivyofanya manaswara kwa mwana wa Maryam. Hakika mimi ni mja. Hivyo semeni “mja wa Allaah na Mtume Wake.”

Ameipokea al-Bukhaariy katika “as-Swahiyh” yake kupitia kwa ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh).

Miongoni mwa maajabu ni kuwa watu wengi ni wachangamfu na ni wenye bidii kuhudhuria sherehe hizi zilizozuliwa na kuzitetea na wanakwepa yale ambayo Allaah ameyawajibisha juu yao katika kuhudhuria Ijumaa na swalah za mkusanyiko na kwao wanaona si lolote si chochote. Sambamba na hilo hawaoni kuwa wanafanya maovu makubwa. Bila shaka hilo ni kutokamana na udhaifu wa imani na uchache wa elimu na madoa mengi yaliyoko kwenye nyoyo miongoni mwa aina mbali mbali ya madhambi na maasi. Tunamuomba Allaah atupe afya sisi na waislamu wengine.

Miongoni mwa maovu hayo ni kuwa baadhi ya watu wanadhania kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anahudhuria Maulidi. Hii ni batili ilio kubwa kabisa na ujinga mbaya sana. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hatoki kwenye kaburi lake kabla ya siku ya Qiyaamah, hana mawasiliano na mtu yeyote na hahudhurii mikusanyiko yao. Bali atabaki kuwemo ndani ya kaburi lake mpaka siku ya Qiyaamah na roho yake iko katika starehe kubwa kabisa kwa Mola Wake Peponi. Amesema (Ta´ala) katika Suurah "al-Mu´muniyn":

ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ تُبْعَثُونَ

"Kisha hakika nyinyi Siku ya Qiyaamah mtafufuliwa." (23:15)

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Mimi ndio mtu wa kwanza ambaye nitatoka ndani ya kaburi siku ya Qiyaamah, mimi ndio muombezi wa kwanza na ndiye wa kwanza atayepewa uombezi.”

Aayah na Hadiyth hii na nyenginezo zenye maana kama hii zote zinafahamisha kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na maiti wengine watatoka ndani ya makaburi yao siku ya Qiyaamah. Hili ni jambo ambalo wanachuoni wa waislamu wamekubaliana juu yake na hawakutofautiana juu yake.

Inapaswa kwa waislamu kuzinduka kwa mambo haya na kutahadhari na yale yaliyozuliwa na wajinga na Bid´ah na ukhurafi mwingine wenye kufanana na hayo ambayo Allaah hakuteremsha dalili yoyote juu yake.

Kuhusiana na kumswalia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni miongoni mwa ´ibaadah bora kabisa na matendo mema. Allaah (Ta´ala) amesema:

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ ۚ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

"Hakika Allaah na Malaika wake wanamswalia Mtume. Enyi mlioamini mswalieni na msalimieni maamkizi ya amani." (33:56)

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kuniswalia mara moja basi Allaah atamswalia mara kumi.”

Ni jambo limewekwa katika Shari´ah kufanya hivo katika nyakati zote na limekokotezwa zaidi mwisho wa kila swalah. Bali ni jambo la wajibu kwa wanachuoni wote katika Tashahhud ya mwisho katika kila swalah na ni Sunnah iliyokokotezwa mahali pengi. Miongoni mwa sehemu hiyo ni baada ya adhaana, wakati anapotajwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), siku ya Ijumaa na usiku wa kumkia Ijumaa, kama zilivyofahamisha hilo Hadiyth nyingi.

Allaah ndiye mwenye jukumu la kutuwafikisha sisi na waislamu wengine wote katika kuweza kuielewa dini, kuwa imara juu yake na kututunukia

kushikamana na Sunnah na kutahadhari na Bid´ah. Swalah na salaam zimwendee Mtume wetu Muhammad, ahli zake na Maswahabah zake wote.[1]

132. al-Lajnah ad-Daaimah Kuhusu Kusherehekea Maulidi

Swali 132: Ni ipi hukumu ya kusherehekea Maulidi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika mwezi wa Rabiy´ al-Awwal kwa lengo la kumuadhimisha (´alayhis-Swalaatu was-Salaam)?

Jibu: Kumuadhimisha Mtume na kumheshimu inakuwa kwa kuamini yale yote aliyokuja nayo kutoka kwa Allaah na kufuata Shari´ah yake sawa katika ´Aqiydah, maneno, matendo na tabia na sambamba na hilo mtu akaacha kuzusha katika dini. Miongoni mwa mambo yaliyozuliwa katika dini ni kusherehekea Maulidi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Shaykh ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah bin Baaz ana maneno yenye kutosheleza amezungumzia hukumu ya kusherehekea Maulidi ya Mtume.[2]

133. Kusherehekea Maulidi Na Israa´ Na Mi´raaj Kwa Lengo Kudhihirisha Desturi Za Kiislamu

Swali 133: Ni ipi hukumu ya kusherehekea mazazi ya Mtume na usiku wa Israa´ na Mi´raaj kwa lengo la kuwalingania watu katika Uislamu na kudhihirisha nembo za Kiislamu kama inavyoonekana Indonesia?

[11] Uk. 10-12

[2] Uk. 13-14 fatwa 3257

Jibu: Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alilingania katika Uislamu kwa maneno, matendo na kupigana Jihaad katika njia ya Allaah. Hakika yeye ni mjuzi zaidi wa njia ya kulingania katika Uislamu, kuieneza na kudhihirisha nembo zake. Miongoni mwa njia za kulingania kwake na kudhihirisha desturi zake haikuwa kusherehekea mazazi yake wala kusherehekea Israa´ na Mi´raaj. Yeye ndiye ambaye anajua zaidi hadhi ya hilo na kulienzi. Maswahabah zake (Radhiya Allaahu ´anhum) wakafuata mfumo wake katika kulingania katika Uislamu na kuueneza. Wao pi hawakusherehekea hayo. Sherehe hizo hazikujulikana kwa maimamu wakubwa wa Uislamu wenye kuzingatiwa ambao ni Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah (Rahimahum Allaah). Hilo lilijulikana kwa wazushi katika dini na waliovuka mipaka kwayo kama Raafidhwah na makundi mengine ya Shiy´ah na wengineo miongoni mwa wale wasiokuwa na elimu juu ya Shari´ah.

Kusherehekea uliyotaja ni Bid´ah ovu. Inaenda kinyume na uongofu wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), makhaliyfah wake waongofu na maimamu wa Salaf-us-Swaalih waliokuwa katika karne tatu bora (Radhiya Allaahu ´anhum). Imethibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

“Mwenye kuzua katika dini yetu hii yasiyokuwemo atarudishiwa mwenyewe.”

“Mwenye kufanya kitendo kisichokuwa ndani yake dini yetu atarudishiwa mwenyewe.”

“Tahadharini na mambo ya kuzua! Hakika kila kitachozushwa ni Bid´ah na kila Bid´ah ni upotevu.”[3]

[3] Uk. 14-15 fatwa 3323

134. Kufanya Maulidi Ni Halali Au Haramu?

Swali 134: Je, kusoma mazazi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni halali au haramu?

Jibu: Kufanya mazazi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na ya mwingine ni miongoni mwa Bid´ah zilizozushwa. Imethibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

“Mwenye kuzusha katika dini yetu hii yasiyokuwemo atarudishiwa mwenyewe.”[4]

135. Kusherehekea Siku Ya 27 Ramadhaan

Swali 135: Ni ipi hukumu ya kusherehekea usiku wa ishirini na saba Ramadhaan peke yake?

Jibu: Kusherehekea usiku wa ishirini na saba peke yake ni Bid´ah iliyozushwa. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Atakayezusha katika dini yetu hii yasiyokuwemo atarudishiwa mwenyewe.”

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

Kilichowekwa katika Shari´ah ni kuuhuisha [usiku huo] kwa ´ibaadah, swadaqah na kadhalika kama masiku kumi mengineyo.[5]

[4] Uk. 27 fatwa 7360

[5] Uk. 41 fatwa 9761

136. Kupika Chakula Usiku Wa Mi´raaj Na Laylat-ul-Qadr Na Kumtumia Thawabu Maiti

Swali 136: Je, inajuzu kupika chakula na kukusanyika kwa ajili yacho katika usiku wa Mi´raaj na katika Usiku wenye cheo (Laylat-ul-Qadr) na kukituma msikitini ili imamu agawe chakula hicho na kupata thawabu kutokana na ada ilivyo?

Jibu: Haijuzu kukhusisha yale yanayoitwa "Usiku wa Mi´raaj" na "Usiku wenye cheo" kutokana na yaliyotajwa ambapo kunatiliwa umuhimu wa kupika chakula wala kukituma msikitini ili kwacho imamu aweze kualika watu kwa kutarajia maiti aweze kupata thawabu. Hili ni Bid´ah. Inatakikana kuachana nayo na kuacha kushikilia hali maalum au wakati maalum wa kuchinja isipokuwa katika Udhhiyah na hajj. Kila kheri inapatikana kwa kufuata uongofu wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).[6]

137. Imaam Ibn Baaz Kusherehekea Usiku Wa Israa´ Na Mi´raaj

Himdi zote anastahiki Allaah Pekee. Swalah na salaam zimwendee Mtume wa Allaah, kizazi chake na Maswahabah zake.

Amma ba´d:

Ni jambo lisilokuwa na shaka yoyote kuwa Israa´ na Mi´raaj ni katika alama kubwa za Allaah zenye kutolea dalili kufahamisha ukweli wa Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na ukubwa wa manzilah yake mbele ya Allaah (´Azza wa Jall). Vilevile kuna dalili juu ya uwezo wa Allaah na kufahamisha kuwa yuko juu ya viumbe Wake wote (Subhaanah). Allaah (Ta´ala) amesema:

[6] Uk. 41-42 fatwa 4990

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَى الَّذِي بَارَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنْ آيَاتِنَا ۚ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

"Utakasifu ni wa Ambaye Amemchukua mja Wake usiku kutoka *al-Masjid al-Haraam* kwenda *al-Masjid al-Aqswaa* ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake ili Tumuonyeshe baadhi ya ishara Zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia yote daima, Mwenye kuona yote daima." (17:01)

Imepokelewa kwa njia mbali mbali kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba alipandishwa mbinguni na akafunguliwa milango yake mpaka akapita mbingu ya saba. Mola Wake akamzungumzisha kwa yale aliyoyataka na akafaradhisha juu yake swalah tano. Mwanzoni (Subhaanah) alikuwa amemfaradhishia swalah khamsini. Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakuacha kuwa ni mwenye kurejea Kwake na kumuomba uwepesi mpaka akamfanyia zikawa tano. Ni faradhi tano lakini hata hivyo inapokuja katika thawabu ni khamsini; kwa sababu tendo jema moja linalipwa mara kumi – himdi na shukurani njema zote anastahiki Allaah.

Hakukuja katika Hadiyth Swahiyh yoyote yenye kusema kuwa Israa´ na Mi´raaj ilikuwa ni usiku fulani. Kila kilichokuja kulenga usiku maalum hakikuthibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa mujibu wa wanachuoni wa Hadiyth. Allaah ni mwingi wa hekima kwa kuwasawazisha nayo watu. Lau hata kungelithibiti kuwa ni usiku maalum basi isingelijuzu kwa waislamu kukhusisha ndani yake kwa kufanya kitu chochote kile katika ´ibaadah na isingelijuzu kuusherehekea kwa kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake hawakusherehekea na wala hawakufanya kitu maalum siku hiyo. Ikiwa kusherehekea ni kitu kimechowekwa katika Shari´ah basi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) angewabainishia Ummah kwa maneno au vitendo. Lau kungelipitika kitu katika hayo kingejulikana na kuwa wazi na hivyo Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) wangetunukulia. Kwani wametunukulia kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) yale yote ambayo Ummah unayahitajia na hawakupuuzia chochote kinachohusiana na dini. Bali Maswahabah wao wametangulia katika kila kheri. Lau kusherehekea usiku huu ingelikuwa ni kitu kimechowekwa katika

Shari´ah basi wao wangelikuwa ni wa kwanza kutangulia kukifanya. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndio mtu wa kwanza mwenye kuwatakia watu mema. Amefikisha ujumbe wake vile inavyostahiki na akatekeleza amana. Lau kuadhimisha usiku huu na kuusherehekea ingelikuwa ni sehemu katika dini ya Uislamu basi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) asingeghafilika kwacho na asingeweza kuficha hilo. Ilipokuwa hakukupitika kitu katika hayo, basi ikajulikana kuwa kuusherehekea na kuuadhimisha ni kitu kisichokuwa na uhusiano wowote ule na Uislamu. Allaah ameukamilishia Ummah huu dini na kuutimizia neema na akamkemea yule mwenye kuweka Shari´ah katika dini yale ambayo hakuyaidhinisha. Allaah (Ta´ala) amesema:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

“Leo Nimekukamilishieni Dini yenu, na Nimekutimizieni neema Yangu, na Nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe ndio Dini yenu.” (05:03)

أَمْ لَهُمْ شُرَكَاءُ شَرَعُوا لَهُم مِّنَ الدِّينِ مَا لَمْ يَأْذَن بِهِ اللَّهُ ۚ وَلَوْلَا كَلِمَةُ الْفَصْلِ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ ۗ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Je, wanao washirika waliowaamuru Dini yale ambayo Allaah Hakuyatolea kwayo idhini? Na lau si neno la uamuzi [ulokwishapita], bila shaka ingelikidhiwa baina yao; na hakika madhalimu watapata adhabu iumizayo.” (42:21)

Imethibiti kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika Hadiyth ambazo ni Swahiyh akitahadharisha Bid´ah na kuweka wazi kuwa ni upotevu kwa lengo la kuuzindua Ummah kuwaonesha ukhatari wake na kuwaogofya kuyavumbua. al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) ambaye ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Atakayezusha katika dini yetu hii yasiyokuwemo basi atarudishiwa mwenyewe.”

Katika upokezi wa Muslim imekuja:

“Mwenye kufanya kitendo ambacho hamna ndani yake dini yetu atarudishiwa mwenyewe.”

Muslim amepokea katika “as-Swahiyh” yake kupitia kwa Jaabir (Radhiya Allaahu ´anh) ambaye ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akisema katika Khutbah zake siku ya Ijumaa:

“Amma ba´d: Hakika maneno bora kabisa ni Kitabu cha Allaah, uongofu bora ni wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), mambo maovu ni ya kuzua, hakika kila Bid´ah ni upotevu.”

Katika Sunan kumepokelewa kupitia kwa al-´Arbaadhw bin Saariyah (Radhiya Allaahu ´anh) ambaye ameeleza:

“Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitutolea mawaidha makali ambayo yalitikisa mioyo yetu na macho yetu yakatiririka machozi. Tukasema: “Ee Mtume wa Allaah! Kana kwamba ni mawaidha ya kutuaga, basi tuusie.” Ndipo akasema: “Ninakuusieni usikivu na utiifu hata kama mtatawaliwa na mtumwa. Hakika yule atakayeishi katika nyinyi basi atakuja kuona tofauti nyingi. Hivyo basi, jilazimieni na Sunnah zangu na Sunnah za makhaliyfah wangu waongofu baada yangu. Shikamaneni nazo bara bara na mziume kwa magego. Tahadharini na mambo ya kuzua! Hakika kila kitakachozushwa ni Bid´ah na kila Bid´ah ni upotevu.”

Hadiyth zenye maana kama hii ni nyingi.

Imethibiti kutoka kwa Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Salaf-us-Swaalih wakitahadharisha juu ya Bid´ah. Si kwa jengine isipokuwa ni kwa sababu ni nyongeza katika dini na Shari´ah ambayo Allaah hakuiidhinisha. Huko ni kujifananisha na maadui wa Allaah miongoni mwa mayahudi na manaswara ambao wameongeza katika dini zao na kufuata yale ambayo Allaah hakuyapa idhini. Hilo linalazimisha kuutukana Uislamu na kuutuhumu kutokamilika. Ni jambo lenye kujulikana kuwa kufanya hivi ni ufisadi mkubwa na maovu yenye kutia aibu. Isitoshe ni kupingana na maneno ya Allaah (´Azza wa Jall):

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ

“Leo Nimekukamilishieni Dini yenu.” (05:03)

Vilevile ni kwenda kinyume wazi wazi na Hadiyth za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambazo zinatahadharisha Bid´ah na kuwakimbiza watu kwazo.

Tunataraji zile dalili tulizotaja ndani yake mna kutosheleza na ukinaishaji kwa yule mwenye kutaka haki juu ya kutahadharisha Bid´ah hizi na kusherehekea usiku wa Israa´ na Mi´raaj na kutahadharisha nayo na kwamba ni kitu kisichokuwa na uhusiano wowote kabisa na Uislamu.

Pale ambapo Allaah aliwajibisha kutoa nasaha kwa waislamu, kuwabainishia yale aliyoyawekea Shari´ah katika dini na akaharamisha kuficha elimu ndipo nikaonelea kuwazindua ndugu zangu juu ya Bid´ah hii ambayo imeenea katika miji mingi mpaka ikafika kiasi cha kwamba baadhi ya watu wakadhani kuwa ni katika dini. Allaah ndiye mwenye jukumu la kuzitengeneza hali za waislamu wote na kuwatunuku uelewa katika dini na kutuwafikisha sisi na wao kushikamana na haki na kuwa na thabati juu yake na wakati huo huo kuachana na yale yenye kwenda kinyume nayo. Hakika Yeye ndiye mwenye kusimamia na muweza wa hilo.

Swalah na salaam zimwendee mja na Mtume Wake Muhammad, kizazi chake na Maswahabah zake.[7]

138. Imaam Ibn Baaz Kusherehekea Usiku Wa Nifsu Sha´baan

Himdi zote anastahiki Allaah, ambaye ametukamilishia dini na akatutimizia neema. Swalah na salaam zimwendee Nabii na Mtume Wake Muhammad, ambaye ni Mtume wa tawbah na Rahmah.

Amma ba´d:

Allaah (Ta´ala) amesema:

[7] Uk. 45-46

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

"Leo Nimekukamilishieni Dini yenu, na Nimekutimizieni neema Yangu na Nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe ndio Dini yenu." (05:03)

أَمْ لَهُمْ شُرَكَاءُ شَرَعُوا لَهُم مِّنَ الدِّينِ مَا لَمْ يَأْذَن بِهِ اللَّهُ

"Je, wanao washirika waliowaamuru Dini yale ambayo Allaah Hakuyatolea kwayo idhini?" (42:21)

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) ambaye ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Atakayezusha katika dini yetu hii yasiyokuwemo basi atarudishiwa mwenyewe.”

Katika upokezi wa Muslim imekuja:

“Mwenye kufanya kitendo ambacho hamna ndani yake dini yetu atarudishiwa mwenyewe.”

Muslim amepokea katika “as-Swahiyh” yake kupitia kwa Jaabir (Radhiya Allaahu ´anh) ambaye ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akisema katika Khutbah yake siku ya Ijumaa:

“Amma ba´d: Hakika maneno bora kabisa ni Kitabu cha Allaah, uongofu bora ni wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), mambo maovu kabisa ni ya kuzua, hakika kila Bid´ah ni upotevu.”

Aayah na Hadiyth zilizo na maana kama hii ni nyingi sana zenye kutoa dalili ya wazi kabisa kuonyesha kuwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) ameukamilishia Ummah huu dini na kuutimizia neema. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakufa isipokuwa baada ya kufikisha vile inavyostahiki na kuubainishia Ummah maneno na vitendo vyote ambavyo Allaah ameweka katika Shari´ah.

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameweka wazi kuwa kila kitendo na neno kinachozushwa na watu na kukinasibisha katika Uislamu ni Bid´ah

yenye kurudishiwa yule mwenye kuizua. Haijalishi kitu hata kama mtu huyo nia yake itakuwa njema. Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) walijua jambo hili. Hali kadhalika wanachuoni wa Uislamu. Hivyo wakakemea Bid´ah na kutahadharisha nayo. Kila ambaye ameandika juu ya kuadhimisha Sunnah na kukemea Bid´ah ametaja hilo. Miongoni mwao ni kama Ibn Wadhdhwaah, at-Twartwuushiy, Abu Shaamah na wengineo.

Miongoni mwa Bid´ah ambazo zimezushwa na watu ni Bid´ah ya kusherehekea usiku wa Nisfu Sha´baan na kuikhusisha siku hiyo kwa kufunga, jambo ambalo halina dalili inayotegemewa. Kumepokelewa juu ya fadhila zake Hadiyth ambazo ni dhaifu. Hivyo haijuzu kuzitegemea.

Kuhusiana na yaliyopokelewa juu ya fadhila ya kuswali katika usiku wa Nifsu Sha´baan yote yametungwa, kama walivyosema wanachuoni wengi jambo ambalo tutalitaja huko mbele – Allaah akitaka. Hali kadhalika kumepokelewa juu yake mapokezi kutoka kwa baadhi ya Salaf wa Shaam na kwenginepo. Hata hivyo wanachuoni wengi wanaonelea kuwa kusherehekea usiku huo ni Bid´ah na kwamba Hadiyth zilizopokelewa zinazozungumzia juu ya fadhila zake zote ni dhaifu na zingine zimetungwa. Miongoni mwa waliotanabahisha hilo ni Haafidhw Ibn Hajar katika kitabu chake “Latwaaif-ul-Ma´aarif” na wengineo. Hadiyth dhaifu zinafanyiwa kazi katika ´ibaadah ambazo kumethibiti asli yake kwa dalili. Kuhusiana na kitendo cha kusherehekea usiku wa Nifsu Sha´baan ni kitu kisichokuwa na asli sahihi mpaka mtu aweze kuegemea Hadiyth hizo dhaifu. Imaam Abul-´Abbaas Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah ametaja kanuni hii tukufu (Rahimahu Allaah).

Msomaji! Nitakunukulia waliyosema baadhi ya wanachuoni kuhusiana na masuala haya ili uwe katika ubainifu juu ya hilo. Wanachuoni wote (Rahimahumu Allaah) wamesema kuwa lililo la wajibu ni kurudisha masuala yote ambayo watu wametofautiana kwayo katika Kitabu cha Allaah (´Azza wa Jall) na Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Yale yenye kuhukumiwa na hivyo viwili au kimoja wapo, basi hiyo ndio Shari´ah ambayo ni wajibu kuifuata. Yale yenye kwenda kinyume navyo basi ni wajibu kukitupilia mbali. Zile ´ibaadah ambazo hazikuthibiti katika hivyo viwili basi

ni Bid´ah. Hivyo itakuwa haijuzu kukitendea kazi, sembuse kulingania kwacho na kukipendekeza. Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ ۖ فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا

"Enyi mlioamini! Mtiini Allaah na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi. Mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Allaah na Mtume mkiwa mnamwamini Allaah na Siku ya Mwisho. Hivyo ni [njia] bora na matokeo mazuri zaidi." (04:59)

وَمَا اخْتَلَفْتُمْ فِيهِ مِن شَيْءٍ فَحُكْمُهُ إِلَى اللَّهِ

"Na katika jambo lolote lile mlilokhitilafiana ndani yake, basi hukumu yake ni kwa Allaah." (42:10)

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ

"Sema: “Mkiwa mnampenda Allaah basi nifuateni, Atakupendeni Allaah na Atakusameheni dhambi zenu." (03:31)

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

"Basi Naapa kwa Mola wako, hawatoamini mpaka wakufanye wewe ni mwamuzi katika yale wanayozozanabaina yao, kisha wasipate katika nyoyo zao karaha katika yale uliyohukumu na wajisalimishe, kwa kujisalimisha [kikamilifu]." (04:65)

Aayah zilizo na maana kama hii ni nyingi zenye kutoa dalili kuonyesha kuwa ni wajibu kurudisha masuala ya tofauti katika Qur-aan na Sunnah na kuridhia kuhukumiwa navyo na kwamba huo ndio muqtadha wa imani na jambo lililo na kheri kwa waja duniani na Aakhirah na ndio mwisho mwema. Haafidhw Ibn Rajab (Rahimahu Allaah) amesema yafuatayo katika kitabu chake “Latwaaif al-Ma´aarif” kuhusiana na masuala haya:

“Taabi´uun wa Shaam kama Khaalid bin Ma´adaan, Mak-huul, Luqmaan bin ´Aamir na wengineo walikuwa wakiadhimisha usiku wa Nifsu Sha´baan na wakijitahidi ndani yake kuleta ´ibaadah mbali mbali. Watu waliiga kutoka

kwao kuufadhilisha na kuuadhimisha. Imesemekana kuwa walifikiwa na baadhi ya mapokezi kutoka kwa wana wa Israaiyl. Mambo yalipotapakaa katika mji ndipo watu wakawa wametofautiana juu ya hilo. Kuna ambao waliyapokea na wakakubaliana nao juu ya kuyaadhimisha. Miongoni mwao ni kundi kutoka watu wa Baswrah na wengineo. Wanachuoni wengi wa Hijaaz wakakemea kitendo hicho. Miongoni mwao ni ´Atwaa´, Ibn Abiy Mulaykah na amepokea hilo ´Abdur-Rahmaan bin Zayd bin Aslam kutoka kwa wanachuoni wa al-Madiynah. Haya ndio maoni ya watu wa Maalik na wengineo ambao wamesema yote hayo ni Bid´ah. Wanachuoni wa Shaam wametofautiana katika kauli mbili juu ya namna ya kuyaadhimisha:

Mosi: Imependekezwa kuyahuisha kwa pamoja msikitini. Khaalid bin Ma´adaan, Luqmaan bin ´Aamir na wengineo walikuwa wakivaa nguo zao nzuri kabisa na wakipaka wanja na wakisimama msikitini usiku huo. Ishaaq bin Raahuuyah ameafikiana naye kwa hilo na kusema kuwa kusimama msikitini kwa pamoja sio kitendo cha Bid´ah. Amemnukuu Harb al-Karmaaniy katika masuala yake.

Pili: Imechukizwa kukusanyika msikitini kwa ajili ya kuswali, kuimba mashairi na kuomba du´aa. Lakini hata hivyo haikuchukizwa kwa mtu peke yake akasimama na kuswali. Haya ni maoni ya al-Awzaa´iy ambaye alikuwa ni mwanachuoni na mwalimu mkubwa wa watu wa Shaam. Hili ndilo lililo karibu [na haki] – Allaah akitaka... Hakujulikani maoni yoyote kutoka kwa Imaam Ahmad kuhusu usiku wa Nisfu Sha´baan. Kumepokelewa mapokezi mawili kuhusu mapendekezo juu ya kusimama usiku wa ´Iyd. Hata hivyo katika upokezi mmoja hakupendekeza kufanya hivyo kwa pamoja kwa sababu ni jambo ambalo halikupokelewa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake. Katika upokezi mwingine amependekeza hilo kutokana na kitendo cha Taabiy´ mmoja ´Abdur-Rahmaan bin Yaziyd bin al-Aswad. Kadhalika kitendo cha kusimama usiku wa Nisfu Sha´baan hakukupokelewa kitu kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wala Maswahabah zake. Limepokelewa kutoka kwa baadhi ya Taabi´uun kutoka kwa wanachuoni wa Shaam." Nilichokuwa nakusudia kukilenga kutoka katika maneno ya Haafidhw Ibn Rajab (Rahimahu Allaah) nimemaliza kukinukuu.

Katika maneno haya ameweka wazi ya kwamba hakukuthibiti chochote kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake (Radhiya Allaahu ´anhum) kuhusu usiku wa Nifsu Sha´baan.

Kuhusiana na yale aliyochagua al-Awzaa´iy (Rahimahu Allaah) juu ya kupendekeza kwa mtu mmoja mmoja kusimama usiku na Haafidhw Ibn Rajab akachagua maoni haya, ni jambo jipya na maoni dhaifu. Kila kitu ambacho hakikuthibiti kwa dalili ya Qur-aan au Sunnah kuonesha kuwa kimewekwa katika Shari´ah haijuzu kwa muislamu kukizua katika dini ya Allaah, sawa kitu hicho ikiwa kitafanywa na mtu mmoja mmoja au kitafanywa na watu kwa pamoja, sawa ikiwa atakifanya kwa siri au kwa dhahiri. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kufanya kitendo kisichokuwa ndani yake dini yetu atarudishiwa mwenyewe.”

Kuna dalili nyinginezo zenye kufahamisha juu ya kukemea Bid´ah na kutahadharisha juu yake.

Imaam Abu Bakr at-Twartwuushiy (Rahimahu Allaah) katika kitabu chake “al-Hawaadith wal-Bid´ah” amesema yafuatayo:

“Ibn Wadhdhwaah amepokea kutoka kwa Zayd bin Aslam ambaye amesema: “Hatukumkuta yeyote katika Mashaykh zetu na wanachuoni wetu wakitilia umuhimu wowote Nifsu Sha´baan na Hadiyth ya Mak-huul. Hawatofautishi usiku huo na siku nyinginezo.”

Ibn Abiy Mulaykah aliambiwa kuwa Ziyaadah bin Numayriy amesema kuwa thawabu zinazopatikana katika usiku wa Nifsu Sha´baan ni thawabu za usiku wenye cheo (Laylat-ul-Qadr) ambapo akajibu kwa kusema:

“Lau ningelimsikia mwenyewe na mkononi mwangu niko na bakora basi ningemchapa.”

´Allaamah ash-Shawkaaniy (Rahimahu Allaha) amesema katika “al-Fawaaid al-Majmuu´ah” yafuatayo:

“Hadiyth yenye kusema: “Ee Allaah! Hakika mwenye kuswali Rakaa mia moja usiku wa Nifsu Sha´baan, basi asome katika kila Rakaa al-Faatihah na Qul huwaa Allaahu ahad mara kumi atatatuliwa haja zake zote... ”

imetungwa. Katika matamshi yake kuna uwazi kabisa [wenye kuonesha uongo wake] kutokana na zile thawabu ambazo mtu anapata. Isitoshe wapokezi wake ni watu wasiojulikana. Imepokelewa katika njia ya pili na ya tatu ambazo zote zimetungwa na wapokezi wake hawajulikani.”

Amesema tena katika “al-Mukhtaswar”:

“Hadiyth juu ya kuswali Nifsu Sha´baan ni batili.”

Ibn Hibbaan amepokea kupitia ´Aliy ambaye amesema:

“Inapofika usiku wa Nifu Sha´baan, basi simameni usiku wake na mchana wake mshinde hali ya kuwa mmefunga.”

ni dhaifu.

Amesema vilevile katika “al-La-aaliy” Hadiyth iliyopokea ad-Daylamiy na wengine:

“Rakaa mia moja katika Nifsu Sha´baan kwa Ikhlaasw mara kumi.“

imetungwa. Mapokezi yake mengi katika njia zake zote tatu wapokezi wake hawajulikani na ni madhaifu.

Mapokezi yenye kusema:

“Kuswali Rakaa kumi na mbili kwa Ikhlaasw mara thalathini”

yametungwa.

Mapokezi yenye kusema:

“Kuswali Rakaa kumi na nne.”

yametungwa.

Kuna wanachuoni wa Fiqh na wafasiri wa Qur-aan ambao wamedanganyika na Hadiyth hizi. Miongoni mwao ni mtunzi wa kitabu “al-Ihyaa´” [al-Ghazaaliy] na wengineo. Wamepokea kuhusu swalah katika usiku huu wa Laylat-ul-Qadr kwa njia mbali mbali/au zenye kutofautiana ambazo zote ni batili na zimetungwa. Hili halipingani na upokezi wa at-Tirmidhiy kupitia Hadiyth ya ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) ambapo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alienda al-Baqiy´ na kwamba Mola anateremka katika mbingu ya dunia usiku wa Nifsu Sha´baan na kwamba anasamehe zaidi ya idadi ya manyoa ya ngamia. Sisi tunachozungumzia ni swalah zilizozuliwa katika usiku huu. Pamoja na kwamba vilevile Hadiyth hii ya ´Aaishah ina udhaifu na mkato. Vilevile Hadiyth ya ´Aliy ambayo tumetangulia kuitaja juu ya kusimama usiku huu haipingani na kule kuonyesha kuwa swalah hii imezuliwa kutokana na kasoro inayopatikana ndani yake kutokana na tuliyoyataja.” Mwisho wa kunukuu kile tulichokilenga.

Haafidhw al-´Iraaqiy amesema:

“Hadiyth juu ya kuswali usiku wa Nifsu Sha´baan amezuliwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na ni kumsemea uongo.”

Imaam an-Nawawiy amesema katika kitabu chake “al-Majmuu´”:

“Swalah inayojulikana kama “Swalah ya Raghaaib”ambayo inaswaliwa Rakaa kumi na mbili kati ya Maghrib na ´Ishaa usiku wa kwanza wa Ijumaa Rajab na kuswali usiku wa Nifsu Sha´baan Rakaa mia moja, swalah hizi mbili ni Bid´ah munkari. Mtu asidanganyike na kuona zimetajwa katika kitabu “Quut al-Quluub” na “al-Ihyaa´ Uluum-id-Diyn” na Hadiyth nyinginezo zilizotajwa. Yote hayo ni batili. Mtu asidanganyike na baadhi ya maimamu ambao ziliwatatiza hukumu zake na wakaandika juu ya kuzipendekeza. Wamekosea katika hayo.”

Shaykh Imaam Abu Muhammad ´Abdur-Rahmaan Ismaa´iyl al-Maqdisiy ameandika vizuri juu ya kuzibatilisha, kitabu ambacho amefanya vyema na kupatia. Kuna maneno mengi sana ya wanachuoni kuhusu masuala haya. Lau tutanukuu maneno yao yote waliyoyasema juu ya masuala haya basi

yatakuwa marefu. Pengine katika haya tuliyoyataja kuna utoshelezaji na ukinaishaji kwa mwanafunzi.

Aayah, Hadiyth na maneno ya wanachuoni tuliyotangulia kuyataja inapata kumbainikia yule mwenye kutafuta haki ya kwamba kusherehekea usiku wa Nifsu Sha´baan kwa kuswali au siku nyingineyo na kuukhusisha na kufunga ni Bid´ah munkari kwa mtazamo wa wanachuoni wengi. Hilo ni jambo lisilokuwa na asli katika Shari´ah safi. Ni miongoni mwa mambo yaliyozushwa katika Uislamu baada ya karne ya Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum). Yule mwenye kutafuta haki katika masuala haya na mengine anatosheka na Kauli ya Allaah (´Azza wa Jall):

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

"Leo Nimekukamilishieni Dini yenu na Nimekutimizieni neema Yangu na Nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe ndio Dini yenu." (05:03)

na Aayah nyinginezo zenye maana kama hiyo. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kuzua katika dini yetu hii yasiyokuwemo atarudishiwa mwenyewe.”

na Hadiyth nyinginezo zenye maana kama hiyo. Muslim amepokea katika “as-Swahiyh" yake kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) ambaye ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Msiutofautishe usiku wa Ijumaa kwa kusimama kati ya nyusiku zingine na msitofautishe siku hiyo na kufunga kati ya siku nyinginezo. Isipokuwa tu ikiwa ni swawm aliyokuwa akifunga mmoja wenu.”

Lau kufanya kitu maalum katika ´ibaadah kwenye usiku mmoja wapo ingelikuwa ni kitu kinachojuzu basi kufanya hivo usiku wa Ijumaa ilikuwa ni aula zaidi kuliko siku nyinginezo. Kwa sababu hii ndio siku bora kabisa, kutokana na dalili ya Hadiyth zilizopokelewa kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Ilipokuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ametahadharisha kukhusisha siku hiyo kati ya siku zingine kwa kusimama ikawa ni dalili yenye kufahamisha kuwa nyusiku zingine kadhalika zina haki zaidi ya kutojuzu kukhusisha kitu chochote ndani yake kwa kufanya kitu katika ´ibaadah. Isipokuwa kwa kupatikana dalili sahihi yenye kujuzisha kukhusisha.

Pale ilipokuwa usiku wa Laylat-ul-Qadr na nyusiku za Ramadhan ni mambo yaliyowekwa katika Shari´ah kuswali usiku na mtu kufanya bidii Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akaweka wazi hilo na akawasisitiza watu kufanya hivo. Bali yeye mwenyewe alifanya hivo. al-Bukhaariy na Muslim wamepokea ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kusimama Ramadhaan kwa imani na matarajio, basi atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia.”

“Mwenye kusimama Usiku wenye cheo kwa imani na matarajio, basi atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia.”

Lau usiku wa Nisfu Sha´baan au usiku wa Ijumaa ya kwanza Rajab au usiku wa Israa´ na Mi´raaj ingelikuwa ni kitu kimewekwa katika Shari´ah kukhusisha sherehe au kitu katika ´ibaadah basi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) angeliwaelekeza nacho Ummah kitu hicho au angekifanya mwenyewe. Lau angefanya kitu katika hayo basi Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) wangeunukulia Ummah na wasingewaficha nacho. Hakika Maswahabah ndio watu wabora kabisa na wenye kuwatakia watu kheri zaidi baada ya Mitume (´alayhimus-Swalaatu was-Salaam) na (Radhiya Allaahu ´anhum).

Hakika muda si mwingi mmejua kupitia maneno ya wanachuoni ya kwamba hakukuthibiti kitu kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wala Maswahabah zake (Radhiya Allaahu ´anhum) juu ya fadhila za usiku wa Ijumaa ya kwanza Rajab na usiku wa Nifsu Sha´baan. Kwa hivyo ikajulikana kuwa kusherehekea siku hizo mbili ni Bid´ah iliyozushwa katika Uislamu. Hali kadhalika kukhusisha siku hizo kwa kufanya kitu katika ´ibaadah ni Bid´ah iliyokatazwa. Vilevile usiku wa tarehe ishini na saba Rajab, ambao baadhi ya watu wanaamini kuwa ndio usiku wa Israa´ na Mi´raaj, haijuzu kukhusisha siku hiyo kwa kufanya kitu katika ´ibaadah kama

ambavyo haijuzu pia kusherehekea kutokana na dalili zilizotangulia kutajwa. Hali ni namna hii lau ingelijulikana ni siku gani - tusemeje pale ilipokuwa haijulikani kutokana na kauli sahihi ya wanachuoni. Wenye kusema kuwa ni usiku wa tarehe ishirini na saba Rajab maneno yao ni batili na hayana msingi wowote wa Hadiyth Swahiyh.

Allaah ndiye mwenye jukumu la kutuwafikisha sisi na waislamu wengine katika kushikamana na Sunnah na kuwa na uimara juu yake na kutahadhari na yale yenye kwenda kinyume nayo. Hakika Yeye ndiye mwingi Mwenye kutoa na Mkarimu.

Swalah na salaam zimwendee mja na Mtume Wake, Mtume Wetu Muhammad, ahli zake na Maswahabah zake wote.[8]

139. Baba Ameacha Wasia Atolewe Swadaqah Kila Mwaka Nisfu Sha´baan

Swali 139: Baba yangu aliniusia maishani mwangu kutoa swadaqah kwa kiasi na uwezo wangu usiku wa Nisfu Sha´baan kila mwaka. Nilikuwa nikifanya hivo mpaka hii leo pamoja na kuwa baadhi ya watu wananikataza kufanya hivo na kunambia kuwa inaweza kuwa haijuzu. Je, swadaqah hii usiku wa Nisfu Sha´baan inajuzu kutokana na wasia wa baba yangu au haijuzu?

Jibu: Kukhusisha swadaqah hii Nisfu Sha´baan kila mwaka ni Bid´ah isiyojuzu hata kama baba yako amekuusia kufanya hivo. Ni juu yako kutekeleza swadaqah hii lakini usikhusishe kwa kuitoa Nisfu Sha´baan. Itoe kila mwaka katika mwezi wowote ndani ya mwaka pasi na kukhusisha mwezi maalum. Ingawa bora zaidi uitoe katika Ramadhaan.[9]

[8] Uk.46-49

[99] Uk. 52 fatwa 9760

140. Kusoma Aayah Kwa Idadi Maalum Ili Mtu Apate Alichokipoteza

Swali 140: Mtu akipoteza kitu na akasema**:**

إِنَّهُ عَلَىٰ رَجْعِهِ لَقَادِرٌ

"Hakika Yeye juu ya kumrudisha kwake bila shaka ni Muweza." (86:08)

mara mia moja. Je, kitamrudilia alichokipoteza au hapana?

Jibu: Hilo halikuthibiti katika Qur-aan na Sunnah. Vilevile sio katika sababu za kawaida zenye kufanya kilichopotea kikarudi. Ni katika kuitumia Qur-aan kwenye mambo ambayo hayakuteremshwa kwa ajili yake. Isitoshe pamoja na kuweka kiwango cha idadi maalum. Kuweka idadi ya kiwango maalum ni jambo linalokuwa kwa mujibu wa Qur-aan na Sunnah peke yake na si jambo linalojulikana kwa kutumia akili. Hivyo kufanya hivo ni Bid´ah. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kuzua katika dini yetu hii yasiyokuwemo, atarudishiwa mwenyewe.”

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.[10]

141. Kusema “Karrama Allaahu wajhah” Kwa ´Aliy Halina Asli

Swali 141: Ni upi usahihi wa maneno yao:

[10] Uk. 69 fatwa 8821

"´Aliy (Karrama Allaahu wajhah)[11]"?

Jibu: Hakuna asli kwa kukhusisha hilo kwa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh). Huko ni kuvuka mipaka kwa watu wa madhehebu ya Shiy´ah.[12]

142. Kusoma Qur-aan Au al-Burdaa Wakati Wa Kwenda Kuzika

Swali 142: Ni ipi hukumu ya kubeba jeneza na huku kunaimbwa Anaashiyd ya al-Burdaa ya al-Buuswiyriy na kula chakula cha wafiwa?

Jibu: Kusoma Qaswiydah ya al-Burdaa au kitu kingine katika Qur-aan au Anaashiyd mbele ya jeneza ni Bid´ah iliyozushwa. Hivyo imekatazwa. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Mwenye kuzua katika dini yetu hii yasiyokuwemo atarudishiwa mwenyewe."

"Mwenye kufanya kitendo kisichokuwa ndani yake dini yetu atarudishiwa mwenyewe."[13]

143. Maana Ya Kufuru Katika Sifa Za Allaah

Swali 143: Kufuru inakuwa nini katika Sifa za Allaah? Je, kuna tofauti kati ya mjuzi, mkaidi na mwenye kufanya Ta´wiyl katika hayo?

[11] Allaah autukuze uso wake

[12] Uk. 69-70 fatwa 6542

[13] Uk. 72 fatwa 5845

Jibu: Kufuru katika Sifa za Allaah (Ta´ala) ni kule mtu kupinga kitu ambacho kuthibiti kwake kumejulikana baada ya kufikiwa na kufanya Ilhaad kwa kupotosha kilichokusudiwa pasi na kuwepo utata wenye kupewa udhuru kwa ajili yake.

Mwenye kwenda kinyume na haki katika hilo kwa ukaidi baada ya kubainishiwa na kusimamishiwa hoja ni kafiri asiyepewa udhuru.

Kuhusiana na yule mwenye kwenda kinyume katika hilo kwa kufanya Ta´wiyl kutokana na utata, anapewa udhuru kwa mtu kama yeye. Ni mwenye kukosea anapewa udhuru na anapewa ujira kwa Ijtihaad yake.[14]

144. Hadiyth Ya Mjakazi Kuhusu Allaah Kuwa Juu Ni Dhaifu?

Swali 144: Kuthibiti kwa Allaah kuwa juu kutokana na Hadiyth ya mjakazi. Je, Hadiyth hii ni Swahiyh wazi wazi inayosema kuwa:

“Allaah Yuko mbinguni.”?

Imaam al-Ghazaaliy anasema alikuwa alipokuwepo, alikuwepo kabla ya kuumba zama na sehemu. Tunataraji utatuwekea wazi hili.

Jibu: Hadiyth ya mjakazi inayosema kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimuuliza:

“Allaah Yuko wapi?” Akasema: “Mbinguni.” Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akamwambia mmiliki wake: “Mwache huru, kwani hakika ni muumini.”

ni Swahiyh. Kuna dalili juu ya kuthibiti uwepo juu wa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) na kwamba Yuko juu ya viumbe Wake na ametengana na viumbe Wake, jambo hilo limetolewa dalili na kuthibitishwa na Qur-aan na Hadiyth

[14] Uk. 128 fatwa 9272

Swahiyh zilizothibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), maafikiano ya Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) na maimamu wa Salaf (Rahimahumu Allaah) kabla ya kupatikana kwa al-Ghazaaliy. Maoni yake hayazingatiwi wala maoni ya wanachuoni waliokubaliana naye. Lililo la wajibu ni kuamini yaliyothibiti katika Qur-aan na Sunnah, maafikiano ya Maswahabah na maimamu wa Salaf. Tunakuusia usome "al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah" cha Ibn Taymiyyah, "Ijtimaa´ al-Juyuush al-Islaamiyyah" cha Ibn-ul-Qayyim na "al-´Uluw lil-´Aliyy al-Ghaffaar" cha adh-Dhahabiy. Humo mna ubainifu wa haki kwa dalili zake.[15]

145. ´Arshi Na Kursiy Viko Ardhini Au Mbinguni?

Swali 145: ´Arshi na Kursiy vilikuwa wapi; juu ya ardhi au chini ya ardhi?

Jibu: Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaamini kuwa ´Arshi na Kursiy viko juu ya mbingu, mbingu iko juu ya ardhi imeizunguka.[16]

146. Imamu Wa Msikiti Anasema Kuwa Qur-aan Imetengenezwa

Swali 146: Kuna imamu wa msikiti nimemsikia akisoma Hadiyth mwezi huu akizungumzia juu ya fadhila za Qur-aan. Katika maneno yake alisema kuwa Qur-aan ameitengeneza/ameiumba Allaah. Katika kupitia kwangu shule katika somo la Tawhiyd nimepata kujua kuwa Mu´tazilah ndio wenye kusema kuwa Qur-aan imeumbwa na Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wameziponda

[15] Uk. 146-147 fatwa 5275

[16] Uk. 148 fatwa 6648

ponda hoja zao. Kwa sababu Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaamini kuwa Qur-aan haikuumbwa, bali ni Maneno ya Allaah ya kihakika ambayo yameteremshwa kutoka Kwake kumpelekea nayo Muhammad. Mimi sijui kama Shaykh alikuwa na makusudio mengine aliposema hivo au vipi? Unaonaje kuhusiana na maneno aliyosema imamu huyu katika msikiti huyo? Naomba uniwekee wazi.

Jibu: Ikiwa mambo ni kama unavyoamini ya kwamba unaitakidi kuwa Qur-aan ni Maneno ya Allaah ambayo amezungumza kihakika na akamteremshia nayo Muhammad, wewe ni katika Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, upande mwingine imamu wa msikiti amesema kuwa Qur-aan ameitengeneza Allaah, wewe ndiye una ´Aqiydah sahihi inapokuja katika Maneno ya Allaah. ´Aqiydah yako inaafikiana na yale wanayoamini Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

Kuhusiana na maneno ya imamu aliposema kuwa Qur-aan imetengeneza Allaah amekosea kwa kuwa yanaenda kinyume na dalili ya Qur-aan na Sunnah na mfumo wa Salaf katika kuvifahamu. Unaweza kuwasiliana naye na kumzindua. Pengine alisema hivo kwa kuteleza ulimi bila ya kukusudia. Hivyo ajisahihishe na atamke usawa.

Baada ya kuzungumza naye ukiona kuwa anaitakidi kuwa Qur-aan imeumbwa na akaendelea katika I´tiqaad hiyo, mwelekeze katika haki ukiwa na uwezo huo. Vinginevyo mpe kitabu “al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah” na “at-Tadmuriyyah” vya Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) na kitabu “Sharh at-Twahaawiyyah” cha Ibn Abil-´Izz (Rahimahu Allaah). Unaweza vilevile kumwelekeza katika vitabu hivyo akavisome ili aijue ´Aqiydah sahihi.[17]

[17] Uk. 152 fatwa 4106

147. Mwenye Kufa Katika ´Aqiydah Ya Ashaa´irah

Swali 147: Ni ipi hukumu ya mwenye kufa juu ya Tawhiyd ya Ashaa´irah kabla ya kufikiwa na Tawhiyd-ul-Asmaa´ was-Swifaat, hakusikia kwa yeyote na hakuisikia. Lakini hata hivyo amekubali Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah na Tawhiyd-ul-Ilaahiyyah. Hakuna aliyemzindua na kumkataza. Je, mtu huyu anapa udhuru au hapana?

Jibu: Jambo lake liko kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Ashaa´irah sio makafiri. Lakini wamekosea katika kuzifanyia Ta´wiyl baadhi ya Sifa za Allaah.[18]

148. Imaam an-Nawawiy Asiigwe Katika Mlango Huu

Swali 148: Kuna ndugu wanaosema kuwa Imaam an-Nawawiy ni Ash´ariy inapokuja katika Majina na Sifa za Allaah. Je, hili ni sahihi na ni ipi dalili? Je, ni sawa mtu kuwasema vibaya wanachuoni kwa sura kama hii? Wengine wanasema kuwa ana kitabu chenye kuitwa "Bustaan-ul-´Aarifiyn" ambapo amefuata madhehebu ya Suufiyyah humo. Je, maneno haya ni sahihi?

Jibu: Ana makosa katika Sifa za Allaah. Amefuata madhehebu ya wenye kufanya Ta´wiyl na akakosea katika hilo. Hivyo asiigwe katika hilo. Lililo la wajibu ni kushikamana na imani ya Ahl-us-Sunnah ambapo wanathibitisha Majina na Sifa za Allaah zilizothibiti katika Qur-aan na Hadiyth Swahiyh kwa njia inayolingana na Allaah (Jalla wa ´Alaa); bila ya kupotosha, kukanusha, kuziwekea namna wala kuzilinganisha kwa mujibu wa Kauli Yake (Subhaanah):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

[18] Uk. 162 fatwa 6606

"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye Ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)

Kuna Aayah nyinginezo zenye maana kama hiyo.

149. Hukumu Ya Ta´wiyl

Swali 149: Ni ipi hukumu ya kufanya Ta´wiyl kutokana na matamanio ya nafsi?

Jibu: Ni haramu. Inaweza kuwa kufuru na inaweza vilevile kuwa maasi.[19]

150. Idadi Ya Mitume Na Manabii Haijulikani

Swali 150: Kuna idadi ngapi ya Manabii na Mitume (´alayhimus-Swalaatu was-Salaam)?

Jibu: Hakuna anayejua idadi yao. Allaah (Ta´ala) amesema:

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّن قَبْلِكَ مِنْهُم مَّن قَصَصْنَا عَلَيْكَ وَمِنْهُم مَّن لَّمْ نَقْصُصْ عَلَيْكَ

"Na kwa yakini Tumewapeleka Mitume kabla yako; miongoni mwao wako Tuliokusimulia na miongoni mwao wako ambao Hatukukusimulia." (40:78)

Wanaojulikana katika wao ni wale waliotajwa katika Qur-aan au wamesihi kutajwa katika Sunnah.[20]

[19] Uk. 180 fatwa 7916

[20] Uk. 195 fatwa 5611

151. Kwanini Asikufurishwe Anayesema ´Aliy Ndio Mtume?

Swali 151: Tumeona tofauti nyingi katika baadhi ya vitabu ambapo tumesoma ya kwamba ´Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ´anh) ndio Mtume na vitabu vingine vimesema kuwa ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kwamba sio ´Aliy.

Jibu: Mwenye kusema ´Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ´anh) ndio Mtume wa Allaah ni kafiri. Anatakiwa kubainishiwa haki kwa dalili na aelekezwe kuwa Muhammad bin ´Abdillaah ndio Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na sio ´Aliy. Akitubu, ni vizuri, akiendelea mtawala amuue kwa kuwa ameritadi kutoka katika Uislamu.[21]

152. Mtume Alikuwa Macho Israa´ Na Mi´raaj?

Swali 152: Je, Israa´ na Mi´raaj ilikuwa katika hali ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuwa macho au hapana? Je, Mtume alimuona Mola Wake kwa macho yake?

Jibu: Israa´ na Mi´raaj ilipitika hali ya kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) yuko macho, kama ilivyokuja katika dalili za Kishari´ah. Hakumuona (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa macho yake. Hii ndio kauli ya wengi katika Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.[22]

[21] Uk. 263 fatwa 9651

[22] Uk. 266-267 fatwa 3089

153. Mtume Alipandishwa Mbinguni Kwa Roho Bila Ya Mwili Au Vyote Viwili?

Swali 153: Kusafirishwa usiku kwa kupandishwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kutoka msikiti wa al-Aqswaa na kwenda mbinguni ilikuwa ni kwa roho na mwili vikiwa pamoja au ilikuwa ni roho peke yake na ni ipi dalili?

Jibu: Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanasema kuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alisafirishwa usiku kutoka msikiti Mtakatifu usiku na kupelekwa msikiti wa al-Aqswaa kwa roho na mwili wake. Amesema (Ta´ala):

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَى الَّذِي بَارَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنْ آيَاتِنَا ۚ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

"Utakasifu ni wa Ambaye Amemchukua mja Wake usiku kutoka *al-Masjid al-Haraam* kwenda *al-Masjid al-Aqswaa* ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake ili Tumuonyeshe baadhi ya ishara Zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia yote daima, Mwenye kuona yote daima." (17:01)

Neno "mja" limekusanya roho na kiwiliwili vyote pamoja. Kadhalika alisafirishwa kutoka msikiti wa al-Aqswaa na kupandishwa mbinguni (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) akiwa na roho na kiwiliwili. Hilo limethibiti kwa Hadiyth nyingi ambazo amezitaja Ibn Kathiyr na wengine wakati walipokuwa wanaifasiri Aayah hii.[23]

[23] Uk. 267 fatwa 4143

154. Vipi Mtume Aliwaona Watu Motoni Na Qiyaamah Bado?

Swali 154: Hadiyth ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba usiku alipopandishwa [mbinguni] aliona baadhi ya watu Motoni ambao wamefanya madhambi. Vipi hilo na wakati Qiyaamah bado hakijasimama na siku ya hesabu haijafika?

Jibu: Hili ni haki. Ni wajibu kuliamini. Haijuzu kuingia katika mambo ambayo ni kazi ya kipekee ya Allaah (Ta´ala).[24]

155. Mtume (´alayhis-Salaam) Anasahau?

Swali 155: Je, Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anasahau au hasahau?

Jibu: Ndio, inajuzu kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kusahau. Lakini hakubaliwi katika mambo yanayohusiana na Shari´ah, bali Allaah humfunza. al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Ibn Mas´uud (Radhiya Allaahu ´anh) ambaye ameeleza kuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Mimi ni mwanaadamu, ninasahau kama mnavyosahau. Nikisahau nikumbusheni."

Ilikuwa wakati aliposahau katika swalah ya ´Aswr.[25]

[24] Uk. 269 fatwa 9202

[25] Uk. 270 fatwa 6959

156. Maswahabah Kumi Waliobashiriwa Pepo

Swali 156: Ni kina nani waliobashiriwa kuingia Peponi?

Jibu: Waliobashiriwa kuingia Peponi ni wengi. Miongoni mwa Maswahabah ni wale kumi waliotangulia; Abu Bakr, ´Umar, ´Uthmaan, ´Aliy, Twalhah, az-Zubayr, Sa´d bin Abiy Waqqaas, Abu ´Ubaydah bin Jarraah, Sa´iyd bin Zayd na ´Abdur-Rahmaan bin ´Awf.[26]

157. Dini Ya Mayahudi Na Manaswara Haitowanufaisha Kitu

Swali 157: Ni ipi hukumu ya Uislamu juu ya mayahudi na manaswara miongoni mwa wale waliofikiwa na ujumbe wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wakaujua lakini hawakumfuata na badala yake wakafuata dini zao?

Jibu: Wanahesabika ni makafiri na wanataamiliwa matangamano ya makafiri katika hukumu za duniani na Aakhirah. Haitowafaa kitu kushikamana na dini yao ikiwa wanakanusha yale aliyokuja nayo Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).[27]

158. Kupokea Zawadi Kutoka Kwa Makafiri

Swali 158: Vipi tutaamiliane na majirani ambao ni manaswara? Je, wakituletea zawadi tuzipokee? Je, inajuzu kwetu kuwaonyesha nyuso zetu au wakaona zaidi ya uso? Je, inajuzu kwetu kununua kwa wauzaji ambao ni manaswara?

[26] Uk. 288 fatwa 9450

[27] Uk. 298 fatwa 6505

Jibu: Mtendee wema yule mwenye kukutendea wema katika wao hata kama atakuwa ni mnaswara. Akikuletea zawadi ambayo inaruhusiwa mtendee wema kwa zawadi hiyo. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikubali zawadi kutoka kwa kiongozi wa Roma ilihali ni mnaswara. Vilevile alikubali zawadi kutoka kwa mayahudi. Amesema (Ta´ala):

لَّا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُم مِّن دِيَارِكُمْ أَن تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوا إِلَيْهِمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ

"Allaah Hakukatazeni kuwafanyia wema na uadilifu wale wasiokupigeni vita katika Dini na wala hawakukutoeni kutoka majumbani mwenu. Hakika Allaah Anapenda wafanyao uadilifu." (60:08)

Inajuzu kwako [mwanamke] kudhihirisha mbele ya wanawake wao [wa kinaswara] yale ambayo inajuzu kuyaonesha mbele ya wanawake wa Kiislamu katika yale yanayofichwa, mavazi ya mapambo na mfano wa hayo. Hii ndio kauli sahihi zaidi ya wanachuoni. Pia inajuzu kununua kutoka kwao vile mnavyohitajia miongoni mwa vitu vinavyoruhusiwa.[28]

159. Kumuombea Msamaha Maiti Aliyeritadi

Swali 159: Kuna mtu alikuwa ni muislamu kisha akaritadi kutoka katika Uislamu na akafa katika hilo. Je, tunaweza kusema kuwa ni kafiri? Ni ipi hukumu kwa mwenye kuritadi kutoka katika Uislamu? Je, tunaweza kumuombea msamaha kwa Allaah kama kusema "Allaah msamehe dhambi zake?"

Jibu: Ambaye alikuwa muislamu kisha akaritadi ni kafiri. Anatakiwa kuambiwa atubu kwa siku tatu, akitubu ni sawa, la sivyo auawe. Haijuzu kumuombea msamaha akifa katika kuritadi. Amesema (Ta´ala):

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَن يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أُولِي قُرْبَىٰ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ

[28] Uk. 303-304 fatwa 5176

"Haimpasi Nabii na wale walioamini kuwaombea msamaha washirikina japokuwa ni jamaa zao wa karibu baada ya kuwabainikia kwamba wao ni watu wa [Moto wa] ***al-Jahiym."*** **(09:113)**[29]

160. Kuwaombea Msamaha Mababu Waliokufa Katika Shirki

Swali 160: Mimi nina mababu waliokufa juu ya shirki. Je, naweza kuwaombea msamaha au hapana?

Jibu: Haijuzu kwa muislamu kuwaombea msamaha mababu zake wala watu wengine ikiwa wamekufa juu ya shirki. Amesema (Ta´ala):

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَن يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أُولِي قُرْبَىٰ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ

"Haimpasi Nabii na wale walioamini kuwaombea msamaha washirikina japokuwa ni jamaa zao wa karibu baada ya kuwabainikia kwamba wao ni watu wa [Moto wa] ***al-Jahiym." (09:113)***[30]

161. Muislamu Kuanza Kumsalimia Kafiri

Swali 161: Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ametukataza kuanza kuwatolea makafiri Salaam. Je, makatazo haya yanaishia kuwaambia "as-Salaam ´alaykum wa Rahmatullaah" au ni makatazo ambayo kunaingia ndani yake mamkizi aina yote? Je, inajuzu kuanza kumsalimia jirani ambaye ni mnaswara kinyume na kusema "as-Salaam ´alaykum wa Rahmatullaah"

[29] Uk. 304 fatwa 10615

[30] Uk. 305 fatwa 11248

kama kumwambia “Khabari yako”, “Vipi hali yako” au “Khabari ya asubuhi”?

Jibu: Haijuzu kuanza kumtolea kafiri Salaam kutokana na yaliyothibiti kutoka katika Hadiyth ya Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) ambaye ameeleza kuwa Mtume wa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Msianze kuwatolea mayahudi na manaswara Salaam, mkikutana na mmoja wao njiani basi mbane kandoni.”

Ameipokea Muslim.

Anas (Radhiya Allaahu ´anh) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Ahl-ul-Kitaab wakikusalimieni waambieni “wa ´alaykum.”

Wanatakiwa kuitikiwa kutokana na udhahiri wa Hadiyth kwa kuambiwa:

“wa ´alaykum.”

Hata hivyo hakuna ubaya kumsalimia kafiri kwa kumwambia:

“Vipi hali yako”, “Umeamkaje”, “Umelalaje” na mfano wa maamkizi kama hayo kukiwa kuna haja ya kufanya hivo. Hivyo ndivyo wanavyoonelea baadhi ya wanachuoni ikiwa ni pamoja na Abul-´Abbaas Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah).[31]

162. Maiti Humuona Mtume (´alayhis-Salaam) Kaburini?

Swali 162: Mtu akifa na akaingia kaburini anamuona Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)? Je, huambiwa tunayoyasema juu ya mtu huyu ilihali katika wakati mmoja kunaweza kufa watu wengi? Malaika wawili

[31] Uk. 312 fatwa 11123

wanapomuhoji wanamuhoji kwa lugha yake au kwa kiarabu au kwa lugha ya kisirya?

Jibu: Anapofariki mtu na kuzikwa hujiwa na Malaika wawili ambao wanamuuliza juu ya Mola Wake, Mtume wake na dini yake kwa lugha anayoifahamu. Muumini huthibitishwa kuyajibu tofauti na kafiri. Haijalishi kitu hata wakakufa maiti wengi kwa wakati mmoja. Sio jambo la kushangaza. Malaika wana uwezo wasiokuwa nao viumbe.

Kutokana na tunavyojua haikuthibiti kuwa maiti anamuona Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwenye kaburi lake.

Tunakuusia urejee katika kitabu "al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah" cha Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah, "al-Usuwl ath-Thalaathah" cha Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab kuhusiana na mada hii na vitabu vinginevyo kwa ajili ya faida zaidi.[32]

163. al-Lajnah ad-Daaimah Kuhusu "as-Swahiyh" Ya al-Bukhaariy

Swali 163: Ni ipi hukumu ya Uislamu kwa mwenye kupinga Hadiyth ya uombezi ambayo imepokelewa na al-Bukhaariy katika "as-Swahiyh" yake na anaongeza pia kusema kuwa ndani ya "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy kuna Hadiyth za kuundwa?

Jibu: Hakika "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy imekubaliwa na wanachuoni. Hadiyth zake zinategemewa katika kuthibitisha hukumu na kunasimama hoja kwazo kwa mwenye kwenda kinyume. Mwenye kusema kuwa ndani yake kuna Hadiyth za kuundwa ni mjinga mwenye kukosea ambaye ameenda kinyume na maafikiano ya Ummah. Hali kadhalika mwenye kupinga uombezi mkubwa au Hadiyth juu ya maombezi mengine ambazo zimepokea al-

[32] Uk. 324-325 fatwa 9886

Bukhaariy katika “as-Swahiyh” na maimamu wengine wa Hadiyth ni mwenye kwenda kinyume na Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah na Salaf wa Ummah huu. Anafuata madhehebu ya wapindaji na wapotevu.[33]

164. Mtoto Wa Nje Ya Ndoa Ataingia Peponi?

Swali 164: Je, mtoto wa zinaa ataingia Peponi? Imesemekana kuwa mtoto wa zinaa ni najisi na Peponi hakuingii mnajisi.

Jibu: Akifa hali ya kuwa ni muislamu ataingia Peponi. Kuwa kwake mtoto wa nje ya ndoa sio kikwazo. Mtoto wa nje ya ndoa sio najisi. Dhambi ya uzinzi ni kwa yule mzinifu na sio kwa yule aliyeumbwa kwa manii ya zinaa. Amesema (Ta´ala):

وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ

"Na wala mbebaji [wa dhambi] hatabeba mzigo wa mwengine." (17:15)

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Muislamu hanajisiki.”[34]

165. Ibliys Ni Malaika Au Jini?

Swali 165: Je, Ibliys ni katika majini au Malaika?

[33] Uk. 345 fatwa 6747

[34] Uk. 350-351

Jibu: Ibliys ni katika majini na sio katika Malaika. Amesema (Ta´ala):

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ كَانَ مِنَ الْجِنِّ فَفَسَقَ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِ

"Na Tulipowaambia Malaika: “Msujudieni Aadam.” Wakasujudu wote isipokuwa Ibliys alikuwa miongoni mwa majini akaasi amri ya Mola wake." (18:50)

وَخَلَقَ الْجَانَّ مِن مَّارِجٍ مِّن نَّارٍ

"Na Akaumba jini kutokana na mwako wa moto." (55:15)

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

“Malaika wameumbwa kutokamana na nuru, Ibliys ameumbwa kutokamana na ulimi wa moto na Aadam ameumbwa kwa kile mlichoelezwa.”

Ameipokea Muslim.

Hasan al-Baswriy amesema:

“Ibliys hakuwa katika Malaika kabisa. Asli yake ni jini kama jinsi Aadam (´alayhis-Salaam) asli yake ni mwanaadamu.”

Ameipokea Ibn Jariyr kwa mlolongo wa wapokezi kutoka kwake.

Lakini hata hivyo Ibliys alisaliti maumbile. Hilo lilikuwa pale alipokuwa pamoja na Malaika, akajishabihisha nao, akaabudu na kutekeleza ´ibaadah za Hajj pamoja nao. Kwa ajili hiyo ndio maana aliingia katika kuzungumzishwa na wao na akawa ameasi kwa kwenda kinyume na maamrisho ya Allaah ya kusujudu.[35]

[35] Uk. 371 fatwa 7815

166. Qur-aan Au ´Iysaa (´alayhis-Salaam)?

Swali 166: Nimesikia baadhi ya wanachuoni wakisema ni kipi bora; Qur-aan au ´Iysaa bin Maryam

Jibu: Qur-aani maneno ya Allaah hayakuumbwa. ´Iysaa ni mwanaadamu ameumbwa. Alizaliwa na Maryam bint ´Imraan. Hivyo Qur-aan ni bora zaidi.[36]

167. Suurah Za Qur-aan Nani Alizipa Majina?

Swali 167: Ni nani ambaye alizipa majina Suurah za Qur-aan tukufu; ni Mtume au nani?

Jibu: Hatuna andiko kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) lenye kutolea dalili juu ya majina ya Suurah zote. Lakini hata hivyo kumethibiti baadhi ya Hadiyth Swahiyh kuzipa majina baadhi yake kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam); kama mfano wa al-Baqarah na al-´Imraan. Ama Suurah nyinginezo udhahiri ni kwamba zilipewa majina na Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum).[37]

168. Kusoma Na Msahafu Au Bila Msahafu?

Swali 168: Ni ipi bora zaidi; kusoma Qur-aan kwenye msahafu au kusoma bila ya msahafu?

[36] (04/05) fatwa 6093

[37] (04/07) fatwa 2376

Jibu: Bora zaidi ni ile njia ambayo ina manufaa zaidi kwako na kuufanya moyo wako kuwa na khofu zaidi.[38]

169. Kusoma Qur-aan Kwa Sauti Ya Juu Msikitini

Swali 169: Je, inajuzu kusoma Suurah Yaasiyn kwa sauti ya juu msikitini au hapana?

Jibu: Haijuzu kwa yeyote kunyanyua sauti yake kwa kusoma Qur-aan msikitini, si kwa Suurah Yaasiyn wala Suurah nyingine, si ndani ya swalah wala nje ya swalah. Imethibiti kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitoka akawakuta watu wanaswali na wanasoma kwa sauti ambapo akasoma:

“Enyi watu! Kila mmoja wenu anamnong´oneza Mola Wake. Hivyo baadhi wasisome kwa sauti ya juu kwa wengine.”

Isitoshe kufanya hivo kuna kushawishana na kuudhiana.[39]

170. Kuingia Na Msahafu Chooni

Swali 170: Mmoja wetu hubeba msahafu mfukoni mwake na huenda akaingia nao chooni. Ni ipi hukumu ya hilo?

Jibu: Kubeba msahafu mfukoni inajuzu. Haijuzu kwa mtu kuingia chooni ilihali yuko na msahafu. Auweke msahafu sehemu nzuri ili kukiadhimisha na

[38] (04/20) fatwa 9770

[39] (04/24) fatwa 2584

kukiheshimu Kitabu cha Allaah. Lakini akilazimika kuingia nao kwa kuogopa usiibwe lau atauacha nje inajuzu kuingia nao kwa dharurah.[40]

171. Inafaa Kumpa Kafiri Qur-aan Iliyotarjumiwa?

Swali 171: Je, tuna haki ya kumwacha mnaswara kwa lengo la kuongozwa na Allaah akasoma Qur-aan iliyotarjumiwa hata kama atakuwa hana wudhuu?

Jibu: Kulingania katika njia ya Allaah ndio mfumo wa Mitume. Amesema (Ta´ala):

قُلْ هَٰذِهِ سَبِيلِي أَدْعُو إِلَى اللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي ۖ وَسُبْحَانَ اللَّهِ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ

"Sema: “Hii ndio njia yangu nalingania kwa Allaah, juu ya ujuzi mimi na anayenifuata. Na Utakasifu ni wa Allaah - nami si miongoni mwa washirikina".” (12:108)

Kumpa nuskha iliyo na tarjama ya maana ya Qur-aan tukufu ni miongoni mwa aina za kulingania katika dini ya Allaah. Ni sawa kufanya hivo.[41]

172. Kutumia Aayah Za Qur-aan Katika Mazungumzo Ya Kawaida

Swali 172: Ni ipi hukumu ya kutumia Qur-aan wakati mmoja wetu anapofikwa na kitu katika mambo ya dini? Kwa mfano mmoja wetu kusema pale anapofikwa na matatizo au dhiki:

[40] (04/40) fatwa 2245

[41] (04/41) fatwa 2217

تَؤُزُّهُمْ أَزًّا

"Wawachochee kwa uchochezi." (19:83)

Au wakati anapokutana na rafiki yake:

جِئْتَ عَلَىٰ قَدَرٍ يَا مُوسَىٰ

"Kisha ukaja [kwa miadi] ya makadirio ee Muwsaa." (20:40)

Au wakati anapotaka kula:

كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا أَسْلَفْتُمْ فِي الْأَيَّامِ الْخَالِيَةِ

“Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa yale mliyoyatanguliza katika siku nyingi zilopita.”? (69:24)

Na Aayah nyinginezo ambazo zinatumiwa na watu leo.

Jibu: Bora ni kuacha kutumia maneno kama hayo na mfano wake ili kuitakasa Qur-aan na kuilinda na yasiyostahiki.[42]

173. al-Lajnah ad-Daaimah Kuhusu Kusoma Qur-aan Bila Wudhuu

Swali 173: Je, inajuzu kwangu kusoma Qur-aan ikiwa sina janaba lakini hata hivyo sikutawadha? Je, inajuzu kusoma ilihali sikuelekea Qiblah?

Jibu: Inajuzu kusoma Qur-aan kwa asiyekuwa na janaba hata kama hakutawadha na hakuelekea Qiblah. Lakini hata hivyo usiguse msahafu isipokuwa mpaka uwe uko na twahara kutokana na hadathi kubwa na

[42] (04/56) fatwa 3114

ndogo.[43]

174. Kupokea Mshahara Kwa Kufunza Qur-aan

Swali 174: Ni ipi hukumu ya ujira anapewa mwalimu anayewafunza watu Qur-aan?

Jibu: Ni sawa. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anasema:

"Kilicho na haki zaidi kukichukulia ujira kwacho ni Kitabu cha Allaah."[44]

175. Msahafu Wa Zamani Unafanywa Nini?

Swali 175: Niufanye nini msahafu mtukufu ambao makaratasi yake yamechanikachanika?

Jibu: Inajuzu kwako kuufukia kwenye ardhi ya msikiti wowote miongoni mwa misikiti iliyopo. Vilevile inajuzu kwako kuuchoma moto kwa kumuiga ´Uthmaan (Radhiya Allaahu ´anh).[45]

[43] (04/78) fatwa 6505

[44] (04/91) fatwa 4160

[45] (04/98) fatwa 967

176. Msahafu Uliochapishwa Makosa Unafanywa Nini?

Swali 176: Nimepata Qur-aan tukufu ambayo imechapishwa vibaya kwa njia ya mpangilio wa Suurah. Je, inajuzu kusoma ndani yake? Na ikiwa haijuzu mnanishauri kuufanya nini? Niuchome moto au niuweke wapi?

Jibu: Uunguze moto au ufukie sehemu ambayo ni pasafi mbali na wanapopita watu na kutupa taka.[46]

177. Vitabu Vya Dini Visivyotumiwa Vinafanywa Nini?

Swali 177: Qur-aan na vitabu vilivyochanikachanika na ambavyo havitumiwi vinafanywa nini?

Jibu: Kurasa za Qur-aan na vitabu vyenye kuheshimiwa ambavyo ndani yake mna utajo wa Allaah au Hadiyth za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni sawa kuvifukia sehemu ambapo ni pasafi au kuvichoma moto.[47]

178. Kusoma Qur-aan Na Huku Mtu Anafuatilia Mkanda

Swali 178: Mimi kila asubuhi ninasoma Qur-aan na wakati huo huo kunakuwa na mkanda unaosoma Qur-aan. Je, inajuzu kufanya hivo?

Jibu: Ndio, inajuzu kwako kusoma Qur-aan midhali sauti ya mkanda haukushughulishi na kusoma na kuzingatia yale unayoyasoma.[48]

[46] (04/99) fatwa 8381

[47] (04/100-101) fatwa 9850

[48] (04/104) fatwa 3924

179. Kusoma Qur-aan Kwa Kushegama, Kusimama Na Kutembea

Swali 179: Je, inajuzu kusoma Qur-aan tukufu kwa ambaye ameshegama, amesimama au anatembea?

Jibu: Inajuzu kufanya hivo. Asli ni kujuzu. Hakukuthibiti dalili yenye kukataza. Allaah (Ta´ala) amesema akiwasifu werevu:

الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيَامًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ

"Ambao wanamdhukuru Allaah kwa kusimama, na kwa kukaa na kwa kulala ubavuni mwao." (03:191)

Kusoma Qur-aan ni miongoni mwa Dhikr.[49]

180. Inajuzu Kusoma Qur-aan Nyakati Swalah Imekatazwa?

Swali 180: Ni ipi hukumu ya kusoma Qur-aan katika nyakati zilizotajwa kwenye Hadiyth ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)? Amekataza (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuswali swalah ya sunnah wakati jua linapochomoza na wakati linapozama.

Jibu: Kusoma Qur-aan katika nyakati ambazo zimetajwa kwenye swali inajuzu kwa kukosekana dalili yenye kukataza. Asli ni kujuzu kusoma

[49] (04/106) fatwa 7720

kutokana na Shari´ah kusisitiza hilo mpaka kuthibiti dalili yenye kukataza.[50]

181. al-Lajnah ad-Daaimah Kusoma Qur-aan Kwa Pamoja

Swali 181: Ni ipi hukumu ya kusoma Qur-aan kwa pamoja? Ninaomba mnitajie dalili kutoka kwenye Qur-aan au Sunnah.

Jibu: Kusoma Qur-aan ni ´ibaadah na ni miongoni mwa mambo bora kabisa ambayo mtu anajikurubisha kwayo kwa Allaah (Ta´ala). Asli katika utekelezaji wa ´ibaadah ni iwe katika sifa ambayo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake (Radhiya Allaahu ´anhum) walikuwa wakifanya. Haikuthibiti kutoka kwake yeye wala Maswahabah zake ya kwamba walikuwa wakisoma kwa pamoja kwa sauti moja. Bali kila mmoja alikuwa anasoma kivyake au mmoja anasoma na wengine huku wanasikiliza. Imethibiti kutoka kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

"Jilazimieni na Sunnah zangu na Sunnah za makhaliyfah wangu waongofu baada yangu."

"Atakayeuzusha katika dini yetu yasiyokuwemo atarudishiwa mwenyewe."

Katika upokezi mwingine imekuja:

"Atakayefanya ´amali isiyokuwemo katika dini yetu atarudishiwa mwenyewe."

Vilevile imethibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba alimuamrisha ´Abdullaah bin Mas´uud (Radhiya Allaahu ´anh) amsomee Qur-aan ambapo akasema: "Ee Mtume wa Allaah! Nikusomee ilihali imeteremshwa kwako?" Akasema:

[50] (04/110) fatwa 6914

"Hakika mimi napenda kuisikia kutoka kwa mwengine."[51]

182. Kwenda Kwa Mbele Na Kwa Nyuma Wakati Wa Kusoma Qur-aan

Swali 182: Tangu tukingali wadogo tukihifadhi Qur-aan kwenye madaftari tumezowea kusoma tukienda kuliani na kushotoni wakati tunaposoma Qur-aan. Kuzunguka kwetu huku tunahisi kuwa kunaturahisishia kusoma Qur-aan. Kuna baadhi ya ndugu ambao wametupinga na kudai kwamba kitendo hichi ni Bid´ah. Pamoja na hivyo hawana dalili yoyote. Tunaomba mtupe faida na kama ni Bid´ah tuache kufanya hivo.

Jibu: Hakuna neno kutokana na uliyoyasema kwenda kuliani na kushotoni wakati wa kusoma. Kuzunguka huku sio ´ibaadah mpaka mtu aweze kusema kuwa ni kuzusha katika dini. Kufanya hivi ni miongoni mwa mazowea ya baadhi ya watu. Kilichokatazwa ni kuzua katika dini. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Atakayezusha katika dini yetu yasiyokuwemo atarudishiwa mwenyewe."

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.[52]

183. Kusema "Swadaqah Allaahu al-´Adhwiym" Ni Bid´ah

Swali 183: Ni ipi hukumu ya kusema "Swadaqah Allaahu al-´Adhwiym" baada ya kumaliza kusoma Qur-aan?

[51] (04/112-113) fatwa 4394

[52] (04/116) fatwa 7423

Jibu: Kusema "Swadaqah Allaahu al-´Adhwiym" baada ya kumaliza kusoma Qur-aan ni Bid´ah. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), makhaliyfah waongofu, Maswahabah wengine na maimamu wa Salaf (Rahimahumu Allaah) wote hawakufanya hivo pamoja na kuwa wao walikuwa wakisoma sana Qur-aan, kuitilia umuhimu na kuijua zaidi. Hivyo kusema hivo na kulazimiana nalo baada ya kila kisomo ni Bid´ah iliyozuliwa. Imethibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

"Atakayezusha katika dini yetu yasiyokuwemo atarudishiwa mwenyewe."

"Atakayefanya ´amali isiyokuwemo katika dini yetu atarudishiwa mwenyewe."[53]

184. Kubusu Msahafu Ni Jambo Halina Asli

Swali 184: Ninawaona watu waanafanya jambo ambalo katu sijawahi kulisikia wala kuliona [hapo kabla], nalo si jengine ni kuwa wanabusu Qur-aan kama jinsi mtu anavyombusu mwengine.

Jibu: Kitendo cha mtu kubusu msahafu hatujui kuwa kina asli.[54]

185. Inajuzu Kumsikiliza Mwanamke Anayesoma Qur-aan?

Swali 185: Ni ipi hukumu ya kusikia kisomo cha mwanamke kilichorekodiwa?

[53] (04/118) fatwa 3303

[54] (04/122) fatwa 4172

Jibu: Inajuzu kwa wanawake tu kusikiliza. Inajuzu vilevile kwa wanaume ikiwa hilo halitopelekea katika fitina.[55]

186. Inafaa Kwa Mwanamke Kusoma Kwa Sauti Ya Juu?

Swali 186: Je, inajuzu kwa mwanamke kusoma kwa sauti ya juu katika swalah ya Subh, Maghrib na ´Ishaa kama mwanaume au yeye anatakiwa kusoma kwa sauti ya siri?

Jibu: Ikiwa yuko peke yake nyumbani, yuko na Mahram zake au yuko pamoja na wanawake wenzake tu anaweza kusoma kwa sauti ya juu. Akiwaongoza wanawake wenzake katika swalah nyumbani kwake na wako wao wenyewe tu anaweza pia kusoma kwa sauti ya juu.

Ama ikiwa anaswali na pembezoni mwake kuna wanaume ambao ni ajinabi kwake wanasikia sauti yake, bora zaidi asisome kwa sauti ya juu.[56]

187. Mashindishano Ya Qur-aan Kwa Wasichana Mbele Ya Wanaume

Swali 187: Ni ipi hukumu ya kufanya mashindishano ya wasichana ya kusoma Qur-aan tukufu kwa utungo na kwa kuwepo wanaume?

Jibu: Wasichana kusoma Qur-aan kwa utungo kwa kuwepo wanaume haijuzu. Kunachelea juu yao wakafitinishwa naye. Shari´ah imekuja kuziba

[55] (04/126) fatwa 3863

[56] (04/126) fatwa 2634

njia zote zinazopelekea katika haramu.[57]

188. Sunnah Ni Wahiy Kutoka Kwa Allaah

Swali 188: Je, Sunnah ni Wahyi au hapana?

Jibu: Sunnah ni Wahyi kutoka kwa Allaah (Jalla wa ´Alaa) kwenda kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Matamshi yake ni ya (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Imesihi kutoka kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

"Hakiki mimi nimepewa Qur-aan ni mfano wake pamoja nayo."[58]

Mwisho!

[57] (04/127) fatwa 5413

[58] (04/285) fatwa 10842